# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
# OFISI YA RAIS –TAMISEMI.

## HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI.

## SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI.

S.L.P 3014 MOSHI, Simu 0755 011 478, Barua pepe: moshitech@yahoo.com

Kumb. Na …….

Mzazi/mlezi wa .....

S.L.P .....

.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI MOSHI ILIYOKO MANISPAA YA MOSHI, MKOA WA KILIMANJARO.**

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya …… Shule hii ni ya bweni na ni ya mchanganyiko wa wavulana na wasichana kwa kidato cha 1-4. Kidato cha 5&6 ni wavulana pekee. Shule iko umbali wa kilometa tano kutoka Moshi Mjini kando ya barabara Kuu ya Moshi-Arusha. Wanafunzi wanaotokea Arusha kuja shuleni wanaweza kuomba kushushiwa nje ya geti la shule kabla ya kufika Moshi mjini. Usafiri wa magari madogo (hiace/daladala) unapatikana kwa nauli ya Tsh 400 na kwa taxi ni wastani wa Tsh 5000 kutoka kituo kikuu cha mabasi.

   Muhula wa masomo wa kidato cha tano utaanza tarehe 02/07/2018. Mwisho wa mwanao kuripoti shuleni ni tarehe 15/07/2018.
   Aidha, unatakiwa kugharamia safari ya kuja shuleni na pia uhakikishe mwanao ana nauli ya kurudi nyumbani wakati shule itakapofungwa mwishoni mwa kila muhula( Juni na Desemba)

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

2.1 **SARE YA SHULE:**

Mzazi/Mlezi unatakiwa kumnunulia mwanao sare ya shule kama ifuatavyo:

- Suruali mbili nyeusi zenye marinda mawili upande wa kulia na kushoto na zisiwe za kubana. Aina ya kitambaa imeambatanishwa.
- Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- Sweta 1 ya mikono mirefu ya rangi ya “dark blue” yenye shingo ya muundo wa “V”. (angalia uzi ulioambatanishwa). Baadhi ya wanafunzi huja shuleni bila sare ya shule kwa sababu mbalimbali na kuja kuzitafuta huku Moshi. Wanafunzi watakaofanya hivyo, bei ya sare za shule kwenye maduka karibu na shule ni sh 34,000 kwa suruwali 2, sweta 1 ni sh 14,000 na mashati meupe 2 ni sh 15,000.

- Viatu vya ngozi vyeusi jozi 2 vya kufunga kwa kamba na visivyokuwa na visigino virefu wala kuchongoka mbele.
- Soksi nyeusi jozi 2.

- Mkanda mweusi wa ngozi (usiwe na bakoli kubwa).
- Nguo za michezo (i) bukta na T-shirt rangi ya bluu bahari. (ii) raba na viatu vya michezo.
- Traki suti rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa kujisomea usiku (preparation).
- Picha 1 ya passport size aliyopiga akiwa amevaa shati jeupe
- Nguo za kushindia (Shamba dress): suruali ya kijani na T-shirt nyekundu au kijani. Pia anaweza kuvaa T-shirt ya shule kama akipenda (zinauzwa shuleni Tsh.11,000/=). Nguo zozote ambazo hazijatajwa kwenye fomu hii haziruhusiwi shuleni na mwanao akija nazo zitakamatwa.

**2.2. ADA NA MICHANGO YA SHULE.**

- Ada ya shule.....Tsh. 70,000/= ( kwa Mwaka)
- Tahadhari(fedha hairudishwi) ……....Tsh. 5000/=
- Kitambulisho na picha.....Tsh. 6,000/=
- Mchango wa Taaluma.....Tsh 20,000/=(kwa Mwaka)
- Ukarabat I wa samani..... Tsh 15,000/=
- Matibabu .....Tsh 10,000/=( kwa Mwaka)
- Walinzi, wapishi na vibarua wengine…….Tsh 30,000/= ( kwa Mwaka)
- Nembo ya shule …….Tsh 2,000/=

**JUMLA Tsh.158,000/=**

**Malipo yafanyike kwenye akaunti ya shule; MOSHI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL, ACC NO. 4031200138, NMB - NELSON MANADELA BRANCH, MOSHI.**

NB. Baadhi ya wanafunzi sio waaminifu hutumia ada na michango kwa matumizi yao binafsi. Hivyo mzazi/mlezi hakikisha unalipa hela Benki na mwanafunzi aje na Bank-Pay-Slip tu ikiwa imeandikwa jina la mwanafunzi, na iwe halisi sio kivuli (photocopy), Unaweza kulipia katika tawi lolote la NMB lililo karibu nawe. **Hatupokei fadha 'cash'shuleni.**

**2.3 MAHITAJI MENGINE AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO:**

- Gododro la sponji lenye ukubwa wa futi 2½x6. Mto na foronya 2 rangi ya bluu bahari
- Blanket 1 la rangi yeyote, shuka 2 za rangi ya bluu bahari (light blue)
- Chandarua nyeupe ya mviringo kwa ajili ya kujikinga na mbu .(Asije na ya pembe nne)
- Vifaa vya kulia chakula (Bakuli, sahani, kikombe na kijiko). Visiwe vya plastiki.
- Ndoo ya kuogea.
- Vifaa kwa ajili ya usafi wa mwili (dawa ya meno, sabuni ya kuogea, mswaki, rangi ya viatu,brashi, taulo n.k).
- Nguo za ndani za kutosha.
- Scientific calculator.
- Madaftari makubwa (counter books) zisizopungua 06.
- Begi la kubebea daftari na liwe la kuvaa mgongoni. Aliweke alama.
- Mzazi mwenye uwezo amtafutie mwanae vitabu vilivyoorodheshwa kuendana na masomo anayosoma.
- Vifaa vya usafi; Wanafunzi wa PCM walete fyekeo 1, soft broom 1, hard broom 1, squizer1, na chelewa yenye mpini 1. Wanafunzi wa PCB walete reki 1, soft broom 1, hard broom 1, squizer1, chelewa yenye mpini 1. Wanafunzi wa CBG walete jembe 1, soft broom 1, hard broom 1, squizer1, chelewa yenye mpini 1.

- Ream ya karatasi: Wanafunzi wa PCM na PCB walete ream moja ya karatasi nyeupe(photocopier A4) na wanafunzi wa CBG walete ream moja ya karatasi zenye mistari (rulled ream).

**2.4 UTARATIBU WA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI.**

- Wazazi, walezi na ndugu wengine wanaweza kuwatembelea wanafunzi Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi jioni. Mgeni yeyote hataruhusiwa kwenda maeneo ya mabweni. Kukiwa na dharura ambayo inamlazimu mzazi/mlezi aje shuleni siku tofauti, dharura hiyo itashughulikiwa na Mkuu wa shule.

- Endapo kutakuwa na tatizo la msiba, mwanafunzi ataruhusiwa kuhudhuria mazishi ya baba mzazi, mama mzazi,au kaka na dada wa kuzaliwa tu na siyo vinginevyo. Matukio ya msiba na mengine yanapotoke utatakiwa kuwasiliana na uongozi wa shule kupitia simu no. 0755 011 478 au 0716 602 946 wakati wowote wa masaa ya kazi.

**2.5 FOMU ZA KUREJESHA SHULENI.**

- Mwanao aje na fomu hii ya kujiunga na shule (Joining Instruction) ukiwa umejaza kwa usahihi pamoja na fomu zilizoamabatanishwa.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa (kama kipo)
- Nakala ya matokeo ya kidato cha nne(result slip)

**2.5 TAHADHARI:**

Tunza fedha na vifaa vyako uwapo safarini. Epuka kupokea vyakula kutoka kwa mtu usiyemfahamu.

Nakutakia Safari njema na KARIBU SANA SHULE YA UFUNDI MOSHI.

**E.S.KYARA**
**MKUU WA SHULE**

**Nakala:** Katibu Mkuu,
OR - TAMISEMI,
S.L.P. 1923, **DODOMA.**

: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu sayansi, na teknolojia.
S.L.P. 9121, **DAR ES SALAAM**.

: Mkurugenzi,
Manispaa ya Moshi,
S.L.P. 318, **MOSHI.**

Mdhibiti Ubora wa Elimu,
Kanda ya Kaskazini Mashariki,
S.L.P. 460, MOSHI.

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Sheria, kanuni, na taratibu za Shule zimewekwa kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi kuelimika na kumaliza elimu yake kwa utulivu na mafanikio makubwa. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayevunja sheria, kanuni na taratibu hizo kwa makusudi. Hatua hizo ni pamoja na adhabu ndogondogo shuleni, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa. Hivyo ni vyema kila mwanafunzi afuate sheria, kanuni na taratibu hizo kwa kutumia hekima, akili, bidii, utii, busara na uaminifu ili kuepukana na uvunjifu wa sheria, kanuni, na taratibu za shule usiokuwa wa lazima. Aidha, kama mwanao ana historia ya utovu wa nidhamu wa mara kwa mara tunakushauri umtafutie shule ya karibu na makazi yako ili uweze kutoa ushirikiano wa kutosha katika malezi yake akiwa shuleni. Hii itakuepushia gharama za kukuita shuleni mara kwa mara kushughulikia utovu wa nidhamu wa mwanao.

1. **<u>HESHIMA, USAFI NA UTUNZAJI WA MALI YA UMMA.</u>**

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu walimu na wafanyakazi wote na pia wanafunzi wenzake na wanajumuiya wote.
b) Kushiriki katika kazi mbalimbali za shule.
- Kuheshimu ratiba nzima ya shule.

c) Mwanafunzi haruhusiwi:-
   i. Kuvuta sigara, bangi wala madawa ya kulevya
   ii. Kufuga kucha, nywele wala ndevu
   iii. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama suruali ya kubana.
   iv. Kugombana au kupigana,
   v. Kunyoa nywele, mitindo ya kihuni kwa mfano kipara/panki au kusuka.
   vi. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
   vii. Kupaka kucha rangi au kutia nywele dawa.
   viii. Kupaka lipstick au kutinda nyusi na kupaka wanja.

d) Kila mwanafunzi atapangiwa eneo lake la kufanyia usafi kila siku na pia atakuwa na zamu ya kudeki darasa, bwalo la chakula, vyoo, na bweni lake na atatakiwa kufanya usafi kwa wakati uliopangwa.
e) Kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote anapotakiwa na awe tayari kwa ukaguzi wakati wowote.
f) Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote zilizopo shuleni. Mwanafunzi atakaye haribu au kupoteza mali ya shule kwa makusudi au kwa uzembe atawajibika kulipia uharibifu au upotevu huo.

2. **<u>MAHUDHURIO</u>.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria:
(i) Vipindi vyote vya masomo vya darasani.
(ii) Miito na mikutano yote k.m. Roll Calls
(iii) Kutunza muda wa ratiba nzima ya shule.
(iv) Kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(v) kufanya majaribio na mitihani yote atakayopewa. Mwanafunzi ambaye hatafanya majaribio au mitihani bila sababu za msingi atalipishwa ‘ream’ ya karatasi kwa uharibifu wa ‘stationery’ na pia atarudishwa nyumbani kwa utovu wa nidhamu na kutokuzingatia taaluma ambayo ndilo lengo la msingi la yeye kuwa hapa.

3. **(A)MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**
   (i) Wizi
   (ii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa.
   (iii) Matumizi ya kilevi cha aina yeyote.
   (iv) Uvutaji wa sigara, bangi na madawa mengine ya kulevya
   (v) Ubakaji na ulawiti
   (vi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yote yale yanayovunja sheria za nchi
   (vii) Kupigana au kupiga.
   (viii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma,
   (ix) Kudharau Bendera ya Taifa.
   (xi) Kumpa mimba msichana/mwanamke.
   (xii) Kutohudhuria vipindi vya masomo mfululizo bila sababu ya msingi.
   (xiii) Kukataa adhabu.
   (xiv) Kunyanyasa wanafunzi wengine.
   (xv) Kulala nje ya shule bila ruhusa maalumu.
   (xvi) Kuanzisha, kuhamasisha, au kushiriki mgomo na vitendo vya uvunjifu wa amani, fujo au kufanya maandamano yasiyokuwa halali/kibali.
   (xvii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi, radio, ipad au camera katika mazingira ya shule.
   (xviii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
   (xix) Kutoa au kushiriki kutoa mimba.
   (xx) Kuharibu mali ya umma kwa maksudi

(B) **<u>MAKOSA MENGINE.</u>**

- Hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila ruhusa.
- Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila sare na ‘gate pass’
- Hairuhusiwi kuingia katika vilabu vya pombe na baa au ‘night clubs’
- Hairuhusiwi kuvaa makoti makubwa , makofia (Boshoro) au mitandio ya kimasai.
- Haituhusiwi kuvaa pete, bangili, hereni, mikufu au kidani.
- Hairuhusiwi kumpeleka mgeni yeyote bwenini aua kumruhusu kulala bwenini.

4. (A) **<u>MABWENI:</u>**
Wanafunzi hawaruhusiwi kupika mabwenini, kutumia pasi za umeme mabwenini au kuwa na ‘heater’. Pia hawaruhusiwi kuunganisha umeme au kutengeneza panapokuwa na hitilafu.

5. **<u>MATIBABU:</u>**
   i. Wagonjwa wanatakiwa kufuata ratiba iliyowekwa ya huduma ya Zahanati ya shule ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.
   ii. Itokeapo dharura ya ugonjwa wakati wa masomo, itamlazimu mwanafunzi kupata kibali cha maandishi cha mwalimu wake ili aweze kutibiwa zahanati.
   iii. Ili kuweza kutibiwa katika hospitali ya Wilaya au Mkoa, mwanafunzi anatakiwa aruhusiwe na Mganga/nesi wa shule na pia kuomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu.
   iv. Kama mwanafunzi amelazwa hospitali ni lazima arudi shuleni mara tu baada ya kuruhusiwa kutoka hospitalini na kuripoti kwa Mkuu wa shule.

v. Shule haina utaratibu wa kuwapa wanafunzi vyakula maalumu (special or light diet) wazazi/walezi wana jukumu la kuona ni jinsi gani watoto wao wenye mahitaji maalumu ya vyakula watakavyohudumiwa.
vi. Mwanafunzi awe na daftari dogo kwa ajili ya matibabu katika zahanati ya shule.
vii. Endapo mwanao ataugua akiwa shuleni kiasi cha shule kutokuweza kumhudumia mzazi utataarifiwa.

**FOMU YA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.**

JINA LA MWANAFUNZI.....
TAREHE YA KUZALIWA.....
JINA LA MZAZI/MLEZI.....
UHUSIANO .....
KAZI YA MZAZI/MLEZI.....

**KIAPO CHA UTII:**

Mimi (Jina la mwanafunzi) .....
Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii nakubali kuwa, Umma wa Nchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia Nchi yangu kwa nguvu zangu zote na kwa uadilifu. Ninaahidi kwa kipindi chote nitakachokuwa katika shule hii nitakuwa mtiifu, sitoshiriki katika mgomo, fujo wala makosa ya jinai. Nitalinda amani na utulivu wa shule kwa njia zozote ikiwemo kutoa taarifa kwa uongozi wa shule kuhusu jambo lolote linalioashiria uvunjifu wa amani shuleni.

Ninajua kuwa serikali inatumia rasilimali zake nyingi kugharamia elimu yangu na mimi ninaahidi kuwa masuala ya taaluma nitayapa kipaumbele cha kwanza ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wasio walimu, na wanafunzi wenzangu wote na kuhudhuria vipindi vyote darasani na kufanaya majaribio na mitihani yote nitakayopewa.

Nikiwa na malalamiko au maoni yoyote nitayafikisha kwa uongozi wa shule kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

Sahihi..... Tarehe.....

**KIAPO CHA MZAZI/MLEZI.**

Mimi mzazi/mlezi wa (jina la mwanafunzi)
……
Ninakiri kuwa nimesoma, nimeelewa na ninakubaliana na sheria , kanuni, na taratibu zote zilizoainishwa za kujiunga na shule hii, na pale mwanangu atakapozikiuka hatua stahili za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Sahihi..... Tarehe.....

## FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

**SEHEMU A:**

1. Jina (MAJINA MATATU)……
2. Tarehe ya kuzaliwa……
3. Utaifa……...Mkoa……Wilaya……...Kabila……
4. **Taarifa ya kubaini wanafunzi Yatima**

   Weka alama ya vema ( √ ) panapohusika.

   (i) Baba na Mama wote walikwishafariki ( )

   (ii) Baba yupo, Mama alikwishafariki ( )

   (iii) Mama yupo Baba alikwishafariki ( )

   (iv) Baba na mama wote wapo ( )
5. Jina la Baba/Mlezi……Kazi yake……..

   Anwani ya Baba/Mlezi……..

   Namba ya simu ya Baba/Mlezi……..

   Anwani ya anakofanyia kazi……..

   .....
6. Jina la Mama/Mlezi…… .Kazi yake……

   Anwani ya Mama/Mlezi……

   .....

   Namba ya simu ya Mama/Mlezi……
7. Je, wazazi wako wanaishi pamoja? Ndiyo/Hapana……...
8. Dini yako……..Dhehebu……
9. Taarifa za maendeleo shuleni zitumwe kwa nani?

   Jina……..Anwani yake……
10. **TAARIFA KUHUSU SHULE ALIYOTOKA MWANAFUNZI**

    (i) Jina la shule …….....

    (ii) Anwani ya shule hiyo .....

    (iii) Namba uliyofanyia mtihani (Index No).....

## ORODHA YA NDUGU/JAMAA WA MWANAFUNZI:

Fomu hii ijazwe na kila mzazi wa mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya Ndugu, Jamaa zake wanne watakaompa huduma mbalimbali mtoto wakati akiwa hapa shuleni. Watakao orodheshwa ndio pekee watapata ridhaa ya kushughulikia masuala ya mwanafunzi awapo shuleni hususani yanapotokea matatizo ya kinidhamu.

| S/N | JINA LA NDUGU/JAMAA | MNAVYOHUSIANA | ANUANI NA NAMBA YAKE YA SIMU | PICHA (PASSPORT SIZE) ZA NDUGU/JAMAA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4. | | | | |

**NATHIBITISHA KUWA TAARIFA HII NI SAHIHI:**

Sahihi ya Mzazi/Mlezi…… Tarehe…….

Sahihi ya Mwanafunzi…….Tarehe…….

**MOSHI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**
**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

To be completed by a Medical Officer (Government hospital)

NAME:……FORM……
……
BLOOD COUNT (Red and White)……
STOOL EXAMINATION……
URINE ANALYSIS……
STAPHILIA TEST……
T.B. TEST……
EYE TEST……
EARS……
CHEST……
SPLEEN……
ABDOMEN……
ADDITIONAL information e.g. Physical defects or impairments……
……
……
Infections, chronic or family diseases etc……

Please certify that the named student above is fit to be enrolled at Moshi Technical Secondary School.

Signature…….

Designation……..

Station……

Date…….

**NB.TO MEDICAL OFFICER:** At the time of examination please TREAT the individual for any ailment you note.

## ORODHA YA VITABU KWA KILA SOMO

### 1. PHYSICS

(I) A lEVEL Physics by Roger Muncaster (4th Edition)
(II) A level Physics by Nelkon and Parker (7th Edition)
(III) A level Physics by Tom Duncan (3rd Edition)

### 2. CHEMISTRY

(i) Organic Chemistry Volume 1
(ii) Advanced level inorganic chemistry Part I & II (TIE 1995)
(iii) Advanced Chemistry review by William W. Davis (Mzumbe Book Project 2004)
(iv) Physical Chemistry by Delungu (Mzumbe Book Project, 1998)

### 3. MATHEMATICS

(I) Advanced Mathematics volume I and II (Ministry of Education and Vocational Training)
(II) Pure mathematics Vol. I & II by Back House
(III) Advanced Mathematics By Tranter and Laube
(IV) The core course for A level by Bastock and Chandler
(V) Advanced Mathematics by Shayo

### 4. GEOGRAPHY

(i) Integrated Approach to physical Geography (Msabila)
(ii) Integrated Geography (By F.J. Monkhouse)
(iii) Map reading for East Africa
(iv) Principles of Geography (By F.J. Monk house)
(v) General Geography in diagram (By R.P. Bunget)
(vi) Simplified Physical Geography for a level (By D.M. Mapunda)

### 5. GENERAL STUDIES

(I) Any General studies Book for "A" Level

### 6. BIOLOGY.

Kitabu kimoja kati ya vifuatavyo;
(i) Biological Science Science 3rd edition.
(ii) Understanding Biology 4th edition.
(iii) Chandi biology class xi (eleven)